

Taswira na Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili vyat KiswahiliZuhura A. Badru¹

Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

Ikisiri

Kwa kuwa fasihi haitoeki katika ombwe, haiwezi kuepuka mabadiliko ya kiutamaduni, kifalsafa na kiujumi. Makala haya yanaangazia suala hili kwa kujikita katika utanzu wa fasihi simulizi, hususan vitendawili. Vitendawili vyat Kiswahili kama sehemu ya fasihi, haviepuki athari za mabadiliko ya kiujumi yanayoikumba jamii ambamo vimeundwa. Mtazamo wa mwandishi wa makala haya ni kuwa thamani ya kiujumi iliyokuwamo katika vitendawili vyat wakati uliopita pamoja na taswira zilizotumika nyakati hizo zina tofauti kubwa na zilizomo katika vitendawili vyat sasa. Kadiri ulimwengu halisi unavyobadilika, tunatarajia pia kuwa thamani ya kiujumi inabadilika na hivyo taswira zinazotumika katika vitendawili zinabadilika ili kuendana na hali hiyo. Mawazo haya ndiyo kiini cha makala haya ambayo yamejikita kwenye mjadala unaohusu taswira na mabadiliko ya kiujumi katika vitendawili vyat Kiswahili. Makala yana jumla ya sehemu tano zilizopangwa kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unatoa picha ya jumla pamoja na kufafanua dhana za msingi kuhusu masuala yanayojadiliwa. Sehemu ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi. Sehemu ya tatu inahusu methodolojia na nadharia ya utafiti. Matokeo ya uchambuzi yamebainishwa katika sehemu ya nne na sehemu tano ni hitimisho.

1.0 Utangulizi

Makala yanahuusutu taswira na mabadiliko ya kiujumi katika vitendawili vyat Kiswahili. Taswira ambayo ni picha ya jambo inayomjia mtu akilini mwake anaposoma au anaposikiliza maelezo fulani zina umuhimu mkubwa katika fasihi. Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) na Badru (2015) taswira huchomozwa na lugha ya picha, ishara pamoja na tamathali za semi kama sitiari na tashibiha. Maelezo haya yanaonesha kuwa ili kupambanua taswira katika kazi ya kifasihi ni lazima kutambua tamathali mbalimbali zilizomo. Katika makala haya mtafiti ameonesha mabadiliko ya kiujumi yalivyoakisiwa kwenye mabadiliko kadhaa ya taswira zilizomo kwenye vitendawili.

¹ Baruapepe: badrulisajr@gmail.com

Kwa upande mwingine, ujumi ni taaluma inayoshughulikia uzuri, ubaya, vionjo hasi au chanya, ubora, udhalili na kufaa au kutookufaa. Aidha, taaluma hii hujenga sheria, kanuni na taratibu zinazotumika katika kushughulikia maswali yanayohusu uzuri na vionjo vya sanaa OUP (2001) na Badru (2015). Wataalamu mbalimbali wamependekeza vigezo vinavyoweza kutumiwa katika kufanya maamuzi ya kiujumi katika sanaa ikiwamo fasihi. Vigezo hivyo ni kama vile utambuzi wa akili, utambuzi wa hisi, utashi wa desturi, uhalisi wa maisha, dhima, umajumui, ulinganisho, utamaduni, uzoefu, ustadi, mwigo na taswira (Dutton, 2009; Lorand, 2000; Haughton, 2004; Leder, 2004; Kant, 2007 na Wamitila, 2008). Vilevile, Wamitila (2008) anaona kuwa hisi, hisia na akili vinategemewa katika kufanya maamuzi ya kiujumi. Hata hivyo, tofauti na ufanuzi wa Wamitila, katika makala haya, mtafiti anaona kuwa vitu hivi vinatakiwa kuhusishwa na taswira kwa sababu kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya maamuzi ya kiujumi na mwitikio wa ishara anazopata msomaji, mtazamaji au msikilizaji wa sanaa fulani.

2.0 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Fasihi na Mabadiliko ya Kiujumi
Fasihi ina sifa ya kuwa hai na jongevu kwa maana ya kwamba inazaliwa, inakua na hata huweza kufa. Vilevile, ni vigumu sana kutenganisha mabadiliko ya kiujumi na mabadiliko katika fasihi ambayo huakisiwa na ubadilikaji wa taswira. Hii ina maana kwamba, jamii inapopitia mabadiliko fulani ya kiujumi, basi na taswira za fasihi ya jamii hiyo hubadilika pia. Katika kujadili suala hili, Kaivola (1996: 10) anahuisha mabadiliko ya kiujumi katika jamii na mabadiliko ya vitendawili kwa kusema:

Vitendawili ni utanu simulizi wa kijadi ambao unajulikana katika tamaduni nyingi. Kasi ya mabadiliko ya kiutamaduni yaliyotokea katika nchi za Magharibi katika miongo michache iliyopita ama imesababisha vifo vya tanzu simulizi za kijadi au kuzitia changamoto ya kubadilika kithamani na kimaana. Muktadha ambamo utamaduni ultendeka na kutumika umebadilika kabisa (Tafsiri yangu).

Ingawa mjadala wa Kaivola unachunguza uhusiano wa sanaa-jadi ikiwamo vitendawili na mabadiliko ya kiujumi katika jamii za Kimagharibi, bado umechochea mjadala wa makala haya kwa kumakinikia jinsi mabadiliko ya jamii yanavyoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili. Vitendawili vya Kiswahili haviepuki athari za mabadiliko haya, ambapo thamani ya kiujumi iliyokuwamo katika vitendawili vya wakati uliopita pamoja na taswira zilizotumika nyakati hizo zina tofauti kubwa na zilizomo katika vitendawili vya sasa.

Wamitila (2008: 62), anapojadili uhusiano baina ya sanaa (katika muktadha huu fasihi) na ujumi, anaonesha wazi akisema:

... inawezakana tathmini ya kiujumi ikaathiriwa na mazingira au utamaduni ambao umemkuza msomaji au anayehusika. Katika vipindi tofauti uamuzi kuhusu kama kazi fulani ina sifa ya urembo au ujumi huweza kutofautiana.

Anaendelea kueleza kuwa maana ya ishara au taswira zilizomo katika kazi ni mojawapo ya sifa za msingi zinazoathiri tathmini ya kiujumi ya yule anayeipokea kazi husika. Msimamo wa Wamitila unatajirisha mjadala wa makala haya kwani anabainisha taswira na ishara kama sifa za msingi katika kutambua thamani ya kiujumi ya kazi husika. Aidha, anasisitiza kuwa kuna uhusiano baina ya mabadiliko ya jamii kiwakati, taswira na kazi ya fasihi inayohusika.

Kwa upande mwingine, Madumulla (1993) anapojadili ukweli wa maisha kama istilahi muhimu ya ujumi, anabainisha aina mbili za ukweli, ambazo ni ukweli halisi na ukweli wa kisanaa. Hapa tunahusika na aina ya pili ya ukweli, yaani ukweli wa kisanaa ambao ni ule wenye kuangalia namna ambavyo ubunifu na matukio halisi hufinyangwa pamoja na kuwasilishwa kwa hadhira. Aidha, maana ya ukweli unaosawiriwa haipatikani kutoka kwa mtunzi, bali kutokana na vigezo vilivyowekwa na jamii husika. Anaendelea kusema kuwa ujumi katika sanaa una wajibu wa kueleza masuala ya kiutu yaliyopo kwa kuzingatia wakati uliopo. Vilevile, anasema kuwa taswira zinazotumika hazina budi kuakisi matukio katika maisha halisi. Kwake, fasihi ni tukio la kihistoria kwa maana ya kwamba inatakiwa kuakisi uhalisi na kutokeza taswira zenye kuakisi matukio yaliyopo pamoja na mabadiliko yake. Akishadidia jambo hili mtaalamu huyu anasema:

Hii inadhihirisha kuwa asili yenye ya fasihi pamoja na tanzu zake ni tukio la kihistoria, ambamo vipengele vyake vyote vyta kazi ya kisanaa pamoja na mwenendo wenye ya kisanaa, na sifa zote za kisanaa hubadilika daima. Hii ina maana kuwa fasihi ni mfumo wa kisanaa wenye uhai na ambao unaguswa sana na mabadiliko ya maisha (Madumula 1993. 144).

Mjadala huu unaohusu uhusiano wa fasihi, ujumi, taswira na mabadiliko ya maisha na ulimwengu kwa jumla umefanyika kwa kina na unatoa mwongozo mzuri katika kujadili uhusiano baina ya taswira na mabadiliko ya kiujumi.

Mawazo haya yanashabihiana na yaliyotolewa na Lema (1993) kuwa fasihi haiwezi kuepuka mabadiliko ya kiutamaduni, kifalsafa na kiujumi na hivyo

watunzi wanatakiwa kuzingatia jambo hili katika utunzi wao. Anaendelea kusisitiza kwamba ujumi huyakinishwa na utamaduni uliopo, yaani mahusiano ya watu katika jamii kwa kuzingatia wakati na mahali. Ingawa mjadala wa Lema ulikusudiwa kwa watunzi wa fasihi andishi, mawazo yake yametupa ari ya kutafiti namna taswira zinavyochangia katika kubainisha mabadiliko ya kiujumi katika vitendawili.

3.0 Methodolojia na Nadharia

Sehemu hii imeshughulikia methodolojia iliyotumika katika upatikanaji wa taarifa za makala haya pamoja na nadharia ilioongoza utafiti ambao ni zao la makala haya.

3.1 Methodolojia

Vitendawili vilivytumika pamoja na data za upili zimepatikana kwa njia ya uchunguzi matini, mahojiano na mjadala wa vikundi baina ya mtafiti na watoataarifa kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Tanga na Mjini Magharibi-Unguja. Data zilizotumika katika makala haya zilikusanywa kwa njia ya mahojiano, uchambuzi wa matini na mjadala ya vikundi.

3.2 Nadharia ya Utafiti

Utafiti uliozaa makala haya pamoja na mjadala wake unaongozwa na mawazo ya Nadharia ya Uhalisia. Hii ni nadharia ambayo inasisitiza juu ya uhusiano baina ya kazi za fasihi na dunia halisi, pamoja na idili na tajiriba za jamii ambamo kazi hizo zimezalishwa. Wahakiki wanaofuata misingi ya nadharia hii wanasisitiza juu ya utunzi wa kazi zinazosawiri na kueleza hali ya maisha kwa kuzingatia uhalisi na uyakinifu. Aidha, wahakiki wa kiuhalisia wanasisitiza suala la ujenzi wa fani na maudhui ya fasihi yanayoakisi hali halisi na mabadiliko ya jamii katika nyanja zote. Mmojawapo wa waasisi wa Nadharia ya Uhalisia, Georg Lukács (1963) ambaye anaamini mambo kadhaa: Kwanza, usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake. Pili, kuchunguza undani wa picha inayoonekana ya uhalisi na kugundua sheria za mabadiliko ya kihistoria zinazosababisha hali fulani. Kwa mujibu wa wafuasi wa nadharia hii, msanii hana budi kuielewa dunia na namna inavyobadilika ili kueleza vizuri mambo yanayojitokeza katika dunia halisi na namna yanavyobadilika.

Hivyo basi, misingi mkuu wa nadharia hii ni kuwa kazi za fasihi zinatakiwa kuzingatia mambo kadhaa ikiwamo: uwasilishaji wa mazingira na maisha ya mwanadamu kiyakinifu, usawiri wa wahusika wenye sifa ya wanadamu wa kawaida wanaoweza kuaminika kwa hadhira, kuakisi mabadiliko ya maisha ya mtu au jamii yake pamoja na kutoa masuluhisho yasiyo ya kinjozi na yanayoweza kutekelezeka (Wamitila, 2003; Ntarangwi, 2004; Wafula na

Njogu, 2007). Kwa ujumla nadharia hii inaona kuwa kazi nzuri ya kifasihi ni ile inayoeleza hali halisi ya ulimwengu pamoja na mabadiliko yake.

4.0 Matokeo ya Utafiti na Uchambuzi wa Data

Katika uchunguzi wetu wa taswira za vitendawili, tumbaini kuwa kwa kadiri dunia inavyopitia mabadiliko ya namna mbalimbali, mwanadamu anatafuta njia mbadala za kuyaeleza na kuyawasilisha mabadiliko hayo, na hivyo anaunda vitendawili vipyta, au kurekebisha vilivyokuwapo kwa minajili ya kuchomoza taswira mpya zenyet kuendana na hali mbadala inayokuwa imejitokeza. Katika makala haya tumbaini kuwa taswira zilizomo kwenye vitendawili vilivyochunguzwa zinaakisi mabadiliko mbalimbali ya kiujumi na kwamba mabadiliko hayo yamejitokeza katika maeneo mbalimbali ya maisha yakiwamo mabadiliko ya kiteknolojia, na kihistoria.

4.1 Mabadiliko ya Kiteknolojia

Kadiri mwanadamu anavyoendelea kuishi anazidi kupata elimu na maarifa mapya yanayomwezesha kuunda vitu mbalimbali vipyta ambavyo hapo awali havikuwapo. Kutohana na kuwa hawezi kuitenga fasihi yake na maendeleo anayopitia, inamlazimu kutunga vitendawili vipyta vyenye kuakisi maendeleo hayo ya kiteknolojia. Kwa mfano:

- (a) Kitendawili: Kilemba cha bibi kinapepea
Jibu: Kibatari
- (b) Kitendawili: Kisimani kwa bibi kuna jini mnywa maji
Jibu: Kibatari
- (c) Kitendawili: Kisimani kwa bibi kuna jini mnywa maji
Jibu: Taa ya kandili
- (d) Kitendawili: Jini wa kisimani kwa bibi akikosa maji hatishi
Jibu: Gari
- (e) Kitendawili: Nina mwanangu ana mbili nyuma, mbili
Jibu: Wanyama wa miguu minne
- (f) Kitendawili: Nina mwanangu ana mbili nyuma mbili mbele
Jibu: Gari
- (g) Kitendawili: Nina gari langu linakwenda mbio kuliko ndege
Jibu: Mawazo
- (h) Kitendawili: Samaki wangu anaenda kimgongomongo
Jibu: Mtumbwi
- (i) Kitendawili: Samaki wangu anaenda kimgongomongo
Jibu: Merikebu
- (j) Kitendawili: Upara wa babu haupigwi konzi
Jibu: Mkuki

- (k) Kitendawili: Kokoliko mlango wa chuma, ukiufungua hauna huruma
Jibu: Bunduki
- (l) Kitendawili: Huingia akiwa amevaa, hutoka uchi
Jibu: Risasi
- (m) Kitendawili: Kuna mti, ukiukunja sauti yake hutisha
Jibu: Bunduki
- (n) Kitendawili: Mwanangu akishiba analia, akiwa na njaa ananyamaza
Jibu: Redio
- (o) Kitendawili: Binadamu anaishi katika sanduku
Jibu: Redio
- (P) Kitendawili: Binadamu anaishi katika sanduku
Jibu: Televisheni
- (q) Kitendawili: Akisema nasikia, nikisema hasikii
Jibu: Redio
- (r) Kitendawili: Tawi langu hodari lanipa habari za dunia
Jibu: Gazeti
- (s) Kitendawili: Kibiriti changu hodari chanioneshaa yaliyoko mbali
Jibu: Runinga
- (t) Kitendawili: Akikosekana maana imekosekana
Jibu: Kamusi
- (u) Kitendawili: Nikitaka kujua neno, namuuliza yeye
Jibu: Kamusi
- (v) Kitendawili: Nikitaka kujua neno, namuuliza yeye
Jibu: Ngamizi
- (w) Kitendawili: Ana akili kupita mtu
Jibu: Ngamizi
- (x) Kitendawili: Kitantalizi mtambua hirizi nitampa dole la ndizi
Jibu: Mtoto aliyeko tumboni
- (y) Kitendawili: Yuko mbali lakini namsikia
Jibu: Mtangazaji wa Redio
- (z) Kitendawili: Yuko mbali lakini namuona
Jibu: Mtangazaji wa runinga

Vitendawili (a), (b) na (c) vinaeleza mabadiliko yaliyotokea katika harakati za mwanadamu kutafuta nishati ambayo inaweza kumkwamua katika kutegemea nishati ya kwanza iliyopatikana kwa kupekecha vijiti. Kutohakana na maendeleo ya teknolojia, mwanadamu amegundua mafuta na kutengeneza vifaa vinavyoweza kutumia mafuta hayo. Hatimaye, ametunga vitendawili vyenye

kubeba taswira zinazoakisi mabadiliko kama yanavyodhihirika katika ulimwengu anamoishi.

Kitendawili (a) kinatupatia taswira ya bibi aliyefunga kilemba na kilemba hicho kinapepea, huku tukipata dhana kuwa kinapepea kwa sababu ya upepo. Kutokana na ujumi wa jamii za Kiafrika na uzoefu wa maisha yao ya kila siku, kitendawili hiki kinapotegwa wanajamii wanaihusisha taswira hiyo na kibatari. Kibatari kinapowaka, moto wake hupepea kuelekea upande mmoja na kuwa mithili ya kilemba. Teknolojia ya wakati huo inadhihirishwa kuititia taswira zilizomo katika kitendawili hiki. Vitendawili (b) na (c) vinaleta taswira ya kisima ambacho ndani yake kuna jini anakunywa maji pasipo kukoma mpaka yaishe. Hata hivyo, ishara zilizotumika (jini mnywa maji na kisima cha bibi) zinachochea taswira tofauti mionganoni mwa hadhira kulingana na uzoefu walionao juu ya ulimwengu wao na mabadiliko waliyopitia, na hivyo kutoa majibu tofauti. Kitendawili kinapotegwa kwa hadhira na muktadha mpya hususan kwenye mazingira na wakati ambapo tayari kuna kandili, jibu lao huwa tofauti na hadhira iliyopitia kipindi cha matumizi ya vibatari. Taswira zilizojitokeza na kusababisha majibu haya zinaakisi mabadiliko yaliyopitiwa na jamii toka matumizi ya vibatari mpaka kutumia taa za kandili. Kizazi cha sasa, kwa kiasi kikubwa, kimepitia mabadiliko makubwa ya kiteknolojia na imekuwa vigumu kwao kutoa jibu la kibatari, kwani hawajakiona, wala kukitumia. Mabadiliko haya ya kiujumi kwa upande wa teknolojia yanadhihirika kuititia taswira zilizojenga kwa kutumia kitendawili hiki.

Kitendawili (d) kwa upande mwengine, kimebadilishwa ili kukidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiteknolojia yaliyowezesha utengenezaji wa magari. Ijapokuwa ishara za *jini* na *kisima* zimetumika kama ilivyokuwa katika vitendawili vilivyotangulia, bado taswira inayojitokeza hapa imerejelea gari na siyo kibatari au taa. Hapa taswira iliyojitokeza ni ya jini ambalo linapokunyuwa maji hutisha (na hata kuweza kufanya madhara), lakini maji yakiisha, halina uwezo huo tena. Katika mazingira anayoishi mwanadamu, gari ni kifaa ambacho hunyonya mafuta na kutokana na hali hiyo gari limefananishwa na jini mnywa maji na yakiisha halifanyi kazi. Vitendawili hivi, kwa pamoja, vina taswira zenye kuakisi mabadiliko ya uhalisi na uzoefu wa jamii hizi kutoka katika matumizi ya vibatari, kwenda katika matumizi ya taa na hatimaye magari.

Vitendawili (e) na (f) navyo vinaonesha namna mabadiliko ya kiteknolojia yanavyoweza kuakisiwa kuititia taswira mbalimbali. Taswira inayojitokeza katika kitendawili (e) inaakisi wanyama wenye miguu minne, ambapo miwili ipo mbele na miwili ipo nyuma. Hata hivyo, katika kitendawili (f) kinachorejelewa ni gari ambalo lina magurudumu ya mbele na ya nyuma.

Taswira ilijojitokeza hapa isingeweza kujitokeza wakati ambapo jamii ilikuwa hajapitia maendeleo na mabadiliko hayo. Hapo awali, wanyama kama vile punda, farasi na ngamia walitegemewa sana katika usafiri wa nchi kavu, hususan kusafirisha watu na mizigo. Baada ya kuweza kutengeneza gari, uzoefu na idili zao zikabadiliwa na hili likaiathiri fasihi yao pia. Mabadiliko haya yanaakiswa kupitia taswira zilizotumiwa katika vitendawili husika.

Kitendawili (g) kinagusia vyombo viwili vya usafiri, ambapo kimoja (gari) kinakwenda kwa kasi kuliko kingine (ndege). Katika ulimwengu halisi, ndege husafiri kwa kasi zaidi ya gari, lakini katika kitendawili hiki, ukiushi umetumika ili kuleta taswira ya kile kinachorejelewa. Katika muktadha huu, taswira inayojitokeza ni ya gari, lakini gari hilo siyo la kawaida kama yalivyo mengine, kwani linaweza kwenda kwa kasi kuliko ndege. Hapa uzuri wa kitendawili hiki unatokana na unyume uliotumika, jambo ambalo linachochea udadisi kwa hadhira katika kuchunguza ulimwengu wake unaoonekana na usioonekana au wa kufikirika ili iweze kupata jibu linaloakisiwa na taswira husika. Kupitia taswira za unyume, kitendawili hiki kinapata ujumi wa kisanaa unaowezesha jibu kupatikana. Katika maisha halisi, mawazo huweza kusafiri kwa kasi sana na kufika mbali ndani ya muda mfupi kuliko chombo chochote cha usafiri. Hata hivyo, kitendawili hiki pamoja na jibu lake visingekuwapo kama mwanadamu angekuwa hajafikia kiwango hiki cha teknolojia.

Vitendawili (h) na (i) navyo vinaakisi mabadiliko ya teknolojia ya vyombo vya usafiri wa majini ambapo matumizi ya mitumbwi yanabadilishana na matumizi ya merikebu. Vitendawili hivi vinapotegwa, mpokezi anaangalia katika maisha yake ya kila siku, uzoefu wake na mazingira halisi yanayomzunguka, na anapata majibu ya vitendawili hivi. Kwa kupitia taswira za vitendawili hivi, mabadiliko ya teknolojia ya vyombo vya usafiri yameasilishwa kwa kadri yanavyopitiwa na dunia.

Vitendawili (j), (k), (l) na (m) vinaibua taswira zinazoakisi mabadiliko katika utengenezaji wa silaha, kutoka zile za jadi mpaka silaha za moto ambazo ni za kisasa zaidi. Kitendawili (j) kinatupatia taswira ya upara ambao mtu hawesi kuupiga konzi. Hata hivyo, kitendawili hiki kimetungwa kwa ukiushi ili kuleta udadisi na kuleta taswira tofauti na iliyozoleka kuhusu upara. Taswira hii yenye ukiushi ndiyo inayoleta uzuri wa kitendawili hiki na kuifanya hadhira ifumbue taswira husika na kupata maana iliyokusudiwa. Mpokezi wa kitendawili hiki analazimika kuhusisha taswira inayojitokeza na vitu anavyovihafamu vyenye sifa zilizotajwa, kisha kuchagua kitu kimoja kinachoshabihiana zaidi na taswira husika. Aidha, mabadiliko haya yanaonesha jinsi fasihi inavyofungamana na utamaduni wa jamii. Kwa mfano, mkuki ni

silaha ya kitamaduni iliyochongoka na kung'aa mithili ya upara, ambayo mtu akijaribu kuipiga konzi ataaumia. Tunapochunguza taswira hii kwa kuihusisha na ujumi uliofungamana na utamaduni wa Kiafrika, tunapata tafsiri mbili. Tafsiri ya kwanza, inachangiwa na utamaduni wa jamii za Waafrika ambapo ‘upara kutokupigwa konzi’, unaashiria juu ya heshima inayoelekezwa kwenye huo upara kwani hapo zamani, aghalabu, wenyе upara/vipara walikuwa ni watu wazima tu, na hasa wazee (ijapokuwa kuna mazingira machache ambapo hata vijana huweza kupata vipara na kwa wengine vipara hivyo husababishwa na maradhi). Hapo awali kitendawili hiki kilisawiri utamaduni wa kuheshimu watu wazima na hivyo watu wasingethubutu kumpiga konzi mzee kutokana na kuheshimu umri wake. Tafsiri ya pili, ni hii inayoakisi mabadiliko yaliyokuwa yamefikiwa na jamii katika teknolojia ya ufuaji chuma na utengenezaji wa silaha. Hapa tunaona kuwa taswira inayojitokeza siyo kuwa inaakisi tu utamaduni wa jamii lakini pia inaakisi maendeleo ya jamii hizi. Aidha, inaonekana kuwa taswira inayojitokeza inafasiliwa kwa namna tofauti kwa kuzingatia ujumi wa jamii hii kwa kipindi husika cha kihistoria na kiteknolojia.

Vitendawili (k), (l) na (m) kwa upande mwingine, vimeundwa kwa kutumia taswira zenye kuonesha mapinduzi ya viwanda vinavyoshughulika na utengenezaji wa silaha. Kitendawili(k) kinachochea hisi za woga na hofu, hasa hadhira inapohusianisha ishara ya mlango wa chuma na bunduki ambayo ikitumika inaleta madhara. Kitendawili (l) kinatumia taswira ya kuonekana ambapo risasi inapokuwa haijatumika huwa na ganda lake na inapotumika hujivua ganda hilo. Kitendawili (m) kinaleta taswira za aina mbili: kwanza, hisi za hofu na woga, na pili, taswira ya kusikika ambapo hadhira inalinganisha mlion wa mti unaokunjwa na mlion wa kutisha wa bunduki/risasi. Kwa ujumla, vitendawili hivi vimebeba taswira zinazowasilisha mabadiliko ya kiteknolojia katika utengenezaji wa silaha, kuanzia katika matumizi ya silaha za jadi, mpaka zile za teknolojia ya juu zaidi.

Mbali na mabadiliko yaliyotokea katika vyombo vyaya usafiri, nishati na utengenezaji wa silaha, jamii imeshuhudia maendeleo katika njia za mawasiliano na habari. Fasihi ya Kiswahili, ukiwamo utanzu wa vitendawili, hauyaepuki mabadiliko haya. Vitendawili (n), (o), (p), (q), (r) na (s) vimeundwa kwa kutumia taswira zinazohusu maendeleo ya vyombo vyaya habari na mawasiliano kama vile magazeti, redio na televisheni. Hapo awali jamii zilitumia mbinu za kiutamaduni katika mawasiliano na kupashana habari kwa kupitia vifaa kama vile ngoma, filimbi, moto na pembe za wanyama. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya ulimwengu kiteknolojia, sasa zinatumika mbinu mpya kama zinavyofafanuliwa katika vitendawili mbalimbali.

Kitendawili (n) kimetungwa kwa unyume ambao dhana ya kushiba inahusishwa na dhana ya kulia, wakati njaa inahusishwa na kunyamaza au kuwa kimya. Taswira inayochomozwa hapa ni ya mtoto anayetenda mambo kinyume na ilivyo kawaida. Unyume huu ndio unaoleta uzuri wa kitendawili hiki na kuichochea hadhira kufumbua taswira husika. Hadhira inapopokea kazi ya fasihi huwa na matarajio fulani kulingana na tajiriba, idili na uzoefu wake, na matarajio hayo yanapofikiwa, au kuwa kinyume chake, humfanya kufikiri zaidi ili kusudi kupata maana ya kazi husika. Katika hali halisi, mtoto akishiba hunyamaa, na akiwa na njaa hulia. Kidokezo hiki huisaidia hadhira kuelewa kuwa mtoto anayetajwa hapa siyo halisi, bali ni taswira ya jambo jingine lililofinyangwa kiubunifu ili kukipa kitendawili hiki uzuri wa kisanaa. Mtoto anayerejelewa hapa ni redio ambayo ikiwa na betri (kushiba) ndipo hutoa sauti, na ikiwa haina (njaa) haitoi sauti.

Vitendawili (o) na (p) kwa upande mwingine, vinatoa taswira zenye kudhihirisha mabadiliko katika mbinu za mawasiliano. Vyote vinatoa taswira ya mtu, lakini mtu huyu si wa kawaida, kwani anaishi sandukuni. Kitendawili kimeundwa kwa kutumia taswira ya sanduku ambayo hurejelea umbo la redio na televisheni. Taswira hizi ndizo zinavipa vitendawili hivi uzuri na hatimaye hadhira kuvipatia maana. Hapa mabadiliko yamedhihirika kutoka katika matumizi ya redio, hadi yale ya televisheni. Vitendawili (q), (r) na (s) navyo vinasawiri mabadiliko katika vyombo vya habari, kuanzia katika magazeti, redio na hata televisheni. Kitendawili (r) kinachochea taswira ya kuonekana ambapo tawi, kutokana na mwonekeno wake, linalinganishwa na gazeti. Hata hivyo, tawi hili siyo tawi la kawaida, kwani lina uwezo wa kuleta habari za dunia. Luga ya picha imetumika na kufinyangwa kiubunifu na hatimaye, kuibua taswira iliyoiwezesha hadhira kupata majibu yanayoakisi tajriba za maisha halisi. Kutokana na mabadiliko, jamii imeunda kitendawili kipyä, yaani kitendawili (s) ili kukifanya kitendawili hicho kiendane na mabadiliko halisi.

Vitendawili (t), (u), (v) na (w) vinahusu mchakato wa mwanadamu katika kutafuta elimu na maarifa juu ya ulimwengu wake na mambo yaliyomo. Kitendawili (u) kilipokuwa kikitegwä hapo awali, kitu kilichokuwa kikijitokeza kama kirejelewa ni kamusi ambayo watu huitumia kupata maelezo ya maneno mbalimbali. Hata hivyo, kutokana na maendeleo yaliyopitiwa na jamii, nafasi ya kamusi kama kirejelewa imechukuliwa na ngamizi (kompyuta) kama inavyojitokeza katika kitendawili (v). Sasa ujumi wa kijamii umebadilika na kwamba jamii inaona ngamizi ni njia bora, nzuri na ya haraka zaidi katika kupata taarifa na maarifa. Kwa kufanya hivyo, ni dhahiri kuwa vitendawili kama utanzu wa kifasihi simulizi una nafasi kubwa ya kuakisi kutumia taswira

thabiti zinazoiwezesha jamii kutambua mabadiliko yanayojitokeza katika mazingira yake halisi.

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, mwanadamu ametengeneza kitu kingine kinachofahamu mambo mengi kuliko mtu mmojammoja. Hii imewezekana kutokana na kukusanya maarifa na uelewa wa watu wengi kwa pamoja na kuutumia sawia. Katika kueleza kushangazwa kwao, wanajamii wametunga kitendawili kinachobeba taswira yenye kuakisi mabadiliko hayo kama inavyodhihirika katika kitendawili (w). Kitendawili hiki kinapotegewa, hadhira inapitia jozi ya vitu inavyovifahamu katika mazingira halisi ambavyo vinaendana na taswira inayojitokeza, na kisha kupata jibu la ngamizi kama kifaa chenye akili kupita mtu.

Kitendawili (x) kimejengwa kwa kutumia taswira ya kuonekana ambapo kuna hirizi, na mtu anatakiwa kuitambua hiyo hirizi. Aidha, kuna ahadi ya zawadi (doe la ndizi) kwa yule atakayeweza kuitambua hirizi. Kwa utamaduni, hirizi huvaliwa kama kinga na haiwekwi wazi kwa kila mtu kuiona, bali hufichwa au kuvaliwa ndani ya nguo. Hili linaashiria kuwa kinachotafutwa kimefichika na ni vigumu kukitambua. Jibu lake ni mtoto aliyeko tumboni ambaye hapo awali ilikuwa vigumu kumtambua ni wa jinsia ipi. Kutokana na mabadiliko katika teknolojia inayohusu huduma ya afya, kitendawili hiki si sahihi na kinapoteza mashiko yake kwani katika uhalisi wa sasa inawezekana kutambua jinsia ya mtoto pasipo kusubiri mtoto azaliwe.

Vitendawili (y) na (z) vinashabihiana kwa kiasi kikubwa na vinadhihirisha mabadiliko ya teknolojia kupitia taswira izipatizo hadhira punde vinapotegewa. Kitendawili (y) “Yuko mbali lakini namsikia”, kinachomoza taswira ya kusikia. Hadhira hujiuliza inawezekanaje mtu akawa mbali, mathalani, nje ya mji ama nchi nyingine lakini akiongea mtu humsikia? Hadhira hupata taswira ya redio ambapo mtangazaji huweza kusikika kutoka mbali. Katika kitendawili (z) mtu si tu kwamba anasikika bali sasa anaonekana. Kitendawili hiki huleta taswira ya kuonekana ambapo watangazaji huonekana na kusikiwa na mtazamaji ijapokuwa wako mbali na mahali alipo mtazamaji. Mabadiliko toka katika kusikia kwenda katika kusikia na kuona yamedhihirishwa kupitia taswira za vitendawili hivi.

Kwa ujumla, vitendawili vinavyoakisi hali mpya za kijamii kwa upande wa teknolojia havikuwapo hapo awali na vimetokea kutokana na mahitaji ya jamii kutaka kuyaeleza matukio mapya na mabadiliko yanayopitiwa na dunia. Mabadiliko ya kiujumi yanapotokea, jamii inatunga fasihi ambayo itakidhi mahitaji yake kulingana na wakati huo. Jamii inaweza kuviachilia mbali baadhi

ya vitendawili na kutunga vinya au kuvitumia vya zamani na kuvipa majibu mapya, kwa kuzingatia taswira mpya zinazochomozwa navyo. Kwa njia hii, jamii inapata fursa ya kuifafanua dunia na mabadiliko yake kwa ufasaha. Katika makala haya mtafiti anatoa hoja kuwa kuna haja ya kuendelea kuvichunguza vitendawili ambavyo kutohana na mabadiliko ya kiujumi havitumiki tena kwani haviendani na mabadiliko yaliyotokea.

4.2 Mabadiliko ya Kihistoria

Vitendawili vinatumika kama njia ya kueleza historia na mabadiliko yake, ambapo vinahifadhi yaliyopita na kueleza yaliyopo na yanayoendelea kutokea. Kutohana na umuhimu wa kueleza mabadiliko ya kihistoria, vitendawili vinabadijika na kuchomoza taswira mpya zinazoweza kuyaeleza mabadiliko hayo. Taswira zinazojitezea katika vitendawili huweza kueleza au kugusia historia ya eneo fulani kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

- (a) Kitendawili: Bibi amelala jalalani
Jibu: Machicha ya nazi
- (b) Kitendawili: Mwarabu katupwa jalalani
Jibu: Machicha ya nazi
- (c) Kitendawili: Mzungu katupwa biwini
Jibu: Machicha ya nazi

Vitendawili hivi vinatoa taswira za kuonekana ambazo zinabadilika kulingana na mabadiliko ya kihistoria yaliyokuwa yakipitiwa na jamii ya Watanzania. Kitendawili (a) kinatoa taswira ya mzee mwanamke akiwa amelala jalalani. Hapa, machicha ya nazi ambayo ni meupe yanalinganishwa na mvi za bibi kizee. Hata hivyo, baada ya ujio wa watawala wa Kiarabu, taswira yake inabadilika kidogo na kuonesha Mwarabu aliyetupwa jalalani pasipo ridhaa yake. Baada ya ujio wa watawala wa Kizungu, kitendawili hiki nacho kinabadilika na taswira inayotokea siyo ya Mwarabu tena, bali Mzungu, kulingana na mabadiliko ya wakati na historia.

Taswira zinazojitezea katika vitendawili (b) na (c) zinabeba kejeli na dhihaka, ambapo watawala waliokuwa wakijihesabu kuwa watu bora sana wanalinganishwa na uchafu au kitu kisicho na thamani. Taswira za vitendawili hivi zinawasilisha ujumbe mzito wa kiti kadi kuwa jamii ya wakati huo ilikuwa na ndoto ya kuuangusha utawala husika kiasi cha kufananishwa na kitendo cha kutupa takataka jalalani. Tunapoangalia ujumi wa vitendawili hivi, tunaona kuwa uzuri na ubaya wake unategemea tofauti baina ya waliotunga vitendawili hivi na wale wanaodhishakiwa. Kwa Waafrika, vitendawili hivi vilikuwa vizuri na viliwafaa kufikisha ujumbe wao wa kutoridhishwa pasipo kukumbana na

hatari ya kudhibitiwa. Kwa upande mwingine, vina ubaya kwa wale waliokuwa wakikejeliwa. Ubora au udhalili wa vitendawili hivi unategemea uhusiano wake na hali halisi iliyopitiwa na jamii ya Watanzania.

Mbali na kuwasilisha hali ya utawala wa kikoloni na mabadiliko yake, taswira za vitendawili zinaakisi pia utawala wa kijadi uliokuwapo kabla ya utawala wa kikoloni. Taswira nyingi zilizojitokeza zinaashiria hisia za watawaliwa juu ya watawala hao kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

- (a) Kitendawili: Kitu kidogo kimemtoa mfalme kitini
Jibu: Haja ndogo
- (b) Kitendawili: Mfalme amekaa chini akina yahe
tumepumzika vitini
Jibu: Boga na majani yake.
- (c) Kitendawili: Bwana Yule kamwangusha Chifu
Jibu: Utelezi

Kitendawili (a) kinachomoza taswira ya mfalme aliyekaa katika kiti chake ambaye, hata hivyo, anatoka katika kiti hicho kwa ajili ya jambo dogo tu. Katika maisha halisi ya wakati huo, mfalme aliheshimiwa na hata wenye shida na mahitaji walimfuata na kumweleza pale alipokaa. Aidha, mfalme alitumikiwa na kufanyiwa kazi na wale waliokuwa chini yake. Ukiushi huu wa kawaida iliyozoleka unasabababisha hadhira kudadisi ni jambo gani, tena dogo linaloweza kumtoa mfalme katika kiti chake. Jibu linalojitokeza ni kuwa tendo la haja ndogo, ijapokuwa ni dogo, ni lazima alitende mwenyewe na hawezি kumwagiza mtu mwingine kumfanya.

Katika kitendawili (b) taswira inayojitokeza ni ya mfalme akiwa amekaa chini, wakati walioko chini ya utawala na mamlaka yake wamekaa vitini wakistarehe. Kwa kawaida, mtawala ni mtu mwenye kuheshimiwa huketi sehemu ya heshima, lakini katika kitendawili hiki taswira inayojitokeza ni kinyume cha kawaida. Unyume huu unakipa kitendawili hiki uzuri na kudhihirisha ubunifu uliotumika katika uundaji wake. Taswira inayojitokeza inashabihiana na mwonekano wa boga linalokuwa chini wakati majani yake yakiwa juu. Kitendawili (c) nacho kinachomoza taswira yenye kuleta hali ya dhihaka. Kwa kawaida, chifu ni mtawala mwenye kuheshimika na hulindwa. Kwa hali hii, ni vigumu mtu kwenda akamwangusha. Kinyume cha matarajio kinaifanya hadhira ifikirie na kutambua ni kitu gani kinachowenza kumwangusha chifu katika maisha halisi. Taswira inayopatikana hapa ni ya kuona ambapo utelezi (kitu kidogo kisicho na heshima) kinamdondosha chifu pamoja na ukuu wake.

Kwa ujumla, vitendawili vilivyocheinuzwa katika sehemu hii ya 4.2 vimetoa taswira zenyé kuakisi mabadiliko mbalimbali ya kihistoria. Kutokana na mabadiliko hayo, jamii imetunga vitendawili vipyä vyenye taswira zinazoakisi mabadiliko ya kihistoria kwa kufuatilia utawala, tangu ule wa kijadi, hadi ule wa kikoloni.

5.0 Hitimisho

Katika makala haya tulidhamiria kujadili mabadiliko ya kiujumi yanavyoakisiwa kupitia vitendawili vya Kiswahili. Katika kutekeleza azma hii tumeonesha jinsi taswira mbalimbali zilizomo kwenye vitendawili zinavyodhihirisha hali halisi ya maisha ya jamii ikiwamo mabadiliko ya kiteknolojia pamoja na maendeleo ya historia. Hatimaye, tumehitimisha kuwa kadiri mabadiliko yanavyotokea, ndivyo vitendawili vipyä vinavyojitokeza au vile vya awali kupata upya kwa minajili ya kuvifanya vitendawili hivyo viendane na hali halisi ya jamii husika. Masuala yaliyojadiliwa kwenye makala haya yanaakisi uthabiti wa msingi mkuu wa Nadharia ya Uhalsia ambapo imeelezwa kwamba mtunzi anatakiwa kuweka juhud za makusudi katika kuwasilisha matukio, watu, mandhari na taswira ambazo zinaoana kwa kiasi kikubwa na hali halisi ya kijamii. Nadharia hii imetufaa kwa kuwa imetuwezesha kuyatambua mabadiliko yaliyomo kwenye jamii na jinsi yalivyoakisiwa kupitia vitendawili.

Marejeleo

- Badru, Z. (2015). *Taswira na Ubainishaji wa Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili*, Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.
- BAKIZA (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Dutton, D. (2009). *The Art Instinct: Beauty, Pleasure and Human Evolution*. Oxford: Oxford University Press.
- Haughton, N. (2004). “Perception of Beauty in Renaissance Art”. In *Journal of Cosmetic Dermatology*. Juz. Na. 3: 229-333. Blackwell Publishing Ltd.
- Kaivola, A. (1966). Riddles and Their Use. In G. Hassan-Rokem & D. Shulman (Eds.), *Untying the Knot: On Riddles and Other Enigmatic Modes*. New York: Oxford University Press.
- Kant, I. (2007). *Critique of Judgment*, Nicholas Walker. (Trans.). New York: Oxford University Press Inc. .

- Lema, E. (1993). "Matatizo ya Waandishi Chipukizi". Katika Mulokozi, M.M na Mung'ong'o, C.G (Wah.), *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji: Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania*. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 59-66.
- Leder, H. (2004). "A model of Aesthetic Appreciation and Aesthetic Judgments". *British Journal of Psychology*, Juz. Na. 95: 489–508.
- Lorand, R. (2000). *Aesthetic Order: A Philosophy of Order, Beauty and Art*. Routledge, London.
- Lukacs, G. (1963). *The Meaning of Contemporary Realism*. Merlin Press, London.
- Madumulla, J.S. (1993). "Waandishi wa Riwaya ya Kiswahili na Suala la Ukweli wa Maisha", Katika Mulokozi, M.M na Mung'ong'o, C.G (Wah.), *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji: Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania*. Dar es Salaam. Kur. 142-153.
- OUP. (2001). *Concise Oxford Dictionary*. 10th ed. London. Oxford University Press.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi. I: Misingi ya Uchaanuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.